# NISHATI
HABARI ZA NISHATI

## News Bulletin

www.nishati.go.tz | Wizara ya Nishati | wizara_ya_nishati_tanzania | @Nishati2017 | Wizara ya Nishati

**Toleo Namba 26** **Mei 1 - 31, 2021**


# WAZIRI MKUU ARIDHISHWA NA KAZI YA UJENZI WA MRADI WA UMEME WA JULIUS NYERERE

- *Awataka wakandarasi kukamilisha mradi kwa wakati*
- *Ataja faida nyingi za mradi*



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa akiwa na Naibu Waziri wa Nishati Wakili Stephen Byabato, Naibu katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Abdul Mahimbali Pamoja na viongozi mbalimbali wakifanya ukaguzi wa ujenzi wa mradi wa kufua umeme kwa maji wa Julius Nyerere (JNHPP) katika maeneo mbalimbali wa mradi huo, Aprili 10, 2021.*


**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI**

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au **Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma**

# WAZIRI MKUU ARIDHISHWA NA KAZI YA UJENZI WA MRADI WA UMEME WA JULIUS NYERERE

**HAFSA OMAR-RUFIJI**



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa ( wa pili kushoto) akimsikiliza Naibu Waziri wa Nishati Wakili Stephen Byabato (katikati) wakati walipokuwa kwenye ziara ya ukaguzi maendeleo ya ujenzi wa mradi wa kufua umeme kwa maji wa Julius Nyerere (JNHPP) Aprili 10, 2021.(kulia) Naibu katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Abdul Mahimbali.

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa amesema ameridhishwa na kasi ya ujenzi wa mradi mkubwa wa kufua Umeme kwa Maji wa Julius Nyerere(JNHPP) unaotekelezwa kwenye mto Rufiji.

Waziri Mkuu ameyasema hayo,Aprili 10,2021, wakati alipofanya ziara ya ukaguzi wa maendeleo wa ujenzi wa mradi huo, ambao utakapokamilika utazalisha umeme wa megawati 2115.

Katika ziara yake hiyo, aliambatana na Naibu Waziri wa Nishati Wakili, Stephen Byabato, Naibu katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Abdul Mahimbali, Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu Edward Ishengoma, Mkurugenzi Mtendaji Tanesco, Dkt. Tito Mwinuka na wataalamu mbalimbali kutoka katika Wizara ya Nishati na Taasisi zake.

Amesema,amefarijika sana kuona kazi nzuri inayofanywa na wakandarasi wa mradi huo, na kuwapongeza viongozi wa Wizara ya Nishati kwa namna ambavyo wanafuatilia, kusimamia na kufanya mradi huo kujengwa kwa kasi ambapo hadi sasa upo kwenye hatua nzuri ya utekelezwaji



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa akiwapungia mikono wafanyakazi mbalimbali (hawapo pichani) wa mradi wa Julius Nyerere (JNHPP) wakati akiwa kwenye ziara ya ukaguzi maendeleo ya ujenzi wa mradi huo, Aprili 10,2021.




## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
**Mhandisi Leonard Masanja**
Katibu Mkuu

**Makamu Mwenyekiti**
**Kheri Mahimbali**

**Mhariri**
**Dorina G. Makaya**

**Waandishi**
Teresia Mhagama
Zuena Msuya
Hafsa Omar

**Msanifu Kurasa**
Lucas Gordon

**Wasiliana nasi kwa simu namba** +255-26-2322018
**Nukushi:** +255-26-2320148
au

**Fika Ofisi ya Mawasiliano**
Mitumba Dodoma,
S.L.P 2494, Dodoma

*www.nishati.go.tz*
*Wizara ya Nishati*
*@Nishati2017*
*wizara_ya_nishati_tanzania*
*Wizara ya Nishati*

# Umeme wa Bwawa la Julius Nyerere kuinua uchumi

Ni matamanio ya kila Mtanzania kupata nishati nafuu ya umeme, pale ujenzi wa Mradi Mkubwa wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) utakapokuwa umekamilika na kuanza uzalishaji.

Matamanio hayo yametiwa bashasha na kauli ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alipofanya ziara kwenye mradi huo Aprili 10 mwaka huu, akifuatana na Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Abdul Mahimbali.

Wengine waliomsindikiza Waziri Mkuu ni Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Edward Ishengoma na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Dk Tito Mwinuka na wataalamu mbalimbali wa Wizara ya Nishati na taasisi zake.

Akiwa hapo, Waziri Mkuu alitaka mradi huo usipotoshwe, kwa kuwa ni wa maji ambao hatimaye utatoa nishati ya umeme nafuu kwa matumizi ya kawaida na ya viwanda, akibainisha kuwa uniti moja itauzwa Sh 36 tu na hata kama kutaibuka gharama nyingine, hautazidi Sh 50.

Hivi karibuni, kumekuwa na kauli kutoka kwa baadhi ya watu zikibeza, kuwa umeme utakaotokana na mradi huo wa kimkakati, hautakuwa endelevu na hivyo kujiandaa kwa shida ya umeme baadaye.

Waziri Mkuu alisisitiza na kutoa ushahidi, kuwa mataifa mengi duniani yanayotumia umeme utokanao na maji watu wao wana unafuu mkubwa, kutokana na umeme huo ambao gharama zake ni ndogo.

Mbali na hilo, wananchi watatumia umeme huo wa uhakika kuendesha shughuli zao za uzalishaji mali katika maeneo mbalimbali viwandani na mashambani, hivyo kuzalisha zaidi na kuchangia uchumi wa nchi.

Kwa hakika kama alivyoshuhudia Waziri Mkuu katika ziara yake, mradi unaendelea vema na ndiyo sababu akaelezea kuridhishwa kwake na kasi ya utekelezaji, kutokana na mkandarasi kulipwa kwa wakati ukitarajiwa kukamilka Juni mwakani.

Kama alivyosisitiza, mradi huo unaendelea kama ilivyopangwa, kwani unaungwa mkono na Serikali, ukizingatiwa ukweli, kwamba mradi huo ni moja ya miradi kipaumbele cha Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Ni dhahiri, kuwa mradi huu utakaozalisha megawati 2,115 utakuwa mkombozi mkubwa kwa Taifa hasa kutokana na mahitaji ya nishati hiyo, ambayo hivi sasa imekuwa ikikumbwa na changamoto mbalimbali za kukatika, na kukwamisha shughuli za uzalishaji kwa baadhi ya watu na taasisi mbalimbali.

Kwa kuwa kuna mradi mwingine wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) ambao nao utahitaji matumizi makubwa ya nishati hiyo ya umeme, ni dhahiri hakutakuwa na matatizo kwa treni za umeme pindi mradi huu utakapokuwa umekamilika.

Ni jukumu na wajibu wa Watanzania kuunga mkono juhudi hizi za Serikali za kutaka kujitegemea katika kujiletea maendeleo ya uchumi, na kuacha kubeza juhudi hizo, ili hatimaye nuru iliyoko mbele ya Taifa kiuchumi, iendelee kung'ara.

# WAZIRI MKUU ARIDHISHWA NA KAZI YA UJENZI WA MRADI WA UMEME WA JULIUS NYERERE

**INATOKA UK.2**

wake kama ambavyo Serikali ilikubaliana na wakandarasi hao.

"Hii ni ziara maalum ya kuja kukagua mwenendo wa mradi wetu wa Julius Nyerere, ambao upo kwenye ujenzi kwa viwango tofauti, kimsingi nimefanya ziara kwenye maeneo sita muhimu kuona mwenendo wake wa ujenzi na hatua iliyofikiwa na nimefurahishwa kuona namna maendeleo ya ujenzi huo yanavyoenda kwa kasi"alisema Waziri Mkuu.

Waziri Mkuu, amewataka wakandarasi wa mradi ,kujenga mradi huo kwa viwango vya kimataifa na utakapo kamilika wanatakiwa kukabidhi mradi ambao utakuwa na ubora na thamani kama walivyokubaliana kwenye mkataba ili mradi uweze kutumika kwa miaka mingi nchini.

Aidha, alisema viongozi wa nchi hii ndio walioamua ujengwe mradi huo mara baada ya kugundua kwamba nchi nyingi zinazotumia umeme wa vyanzo









*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa akiwa na Naibu Waziri wa Nishati Wakili Stephen Byabato, Naibu katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Abdul Mahimbali Pamoja na viongozi mbalimbali wakifanya ukaguzi wa ujenzi wa mradi wa kufua umeme kwa maji wa Julius Nyerere (JNHPP) katika maeneo mbalimbali wa mradi huo, Aprili 10, 2021.*

# WAZIRI MKUU ARIDHISHWA NA KAZI YA UJENZI WA MRADI WA UMEME WA JULIUS NYERERE






*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa akiwa na Naibu Waziri wa Nishati Wakili Stephen Byabato, Naibu katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Abdul Mahimbali Pamoja na viongozi mbalimbali wakifanya ukaguzi wa ujenzi wa mradi wa kufua umeme kwa maji wa Julius Nyerere(JNHPP) katika maeneo mbalimbali wa mradi huo, Aprili 10, 2021.*

vya maji wananchi wake wananufaika kwa kutumia huduma ya umeme wa gharama ndogo na kuwahakikishia watanzania kuwa mradi huo utakamilika kwa wakati.

"Ilimradi Rais wa Jamhuri ya Muungano yupo na sisi wasaidizi bado tupo kutoka ngazi za juu mpaka kwenye Wizara na watendaji wetu nataka niwahakikishie watanzania huu mradi utakamilika kwa wakati kwasababu fedha tunayo, wakandarasi wanafanya kazi yao vizuri, waatalamu wetu wahandisi wanasimamia na shirika letu la umeme Tanesco likiwa ndio jukumu lao kubwa linaendelea kusimamia kwa umakini mkubwa"alisema Mhe. Majaliwa.

Pia, Waziri Mkuu alizitaja faida nyingine za umeme unaozalishwa na vyanzo vya maji, ambapo amesema moja ya faida ya mradi huo ni

# WAZIRI MKUU ARIDHISHWA NA KAZI YA UJENZI WA MRADI WA UMEME WA JULIUS NYERERE



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa akizungumza mara baada ya kumaliza ziara yake ya ukaguzi wa mradi wa kufua umeme kwa maji wa Julius Nyerere (JNHPP) uliopo Rufiji, Aprili 10,2021.*

kuwa umeme unakuwa wa gharama ndogo kulinganisha na umeme wa vyanzo vingine, ambapo ameelezea kuwa gharama ya unit moja itakuwa ni kwa shilingi 36 na alisema kuwa hata kama kutakuwa na gharama nyingine haitazidi shilingi 50.

Ameleeza kuwa, kwa unafuu huo anamini kuwa watanzania wote wataweza kumudu gharama hizo na kuwataka Watanzania kuendelea kuwa na matumaini kwamba umeme wa gharama nafuu unakuja.



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa Pamoja na viongozi mbalimbali wakipata maelezo ya mradi wa mradi wa kufua umeme kwa maji wa Julius Nyerere (JNHPP) kutoka kwa Mha. John M.Mageni (wa pili kulia) ambaye ndio Mhandisi Mkazi wa mradi huo.*

Faida nyingine ya mradi huo, amesema kuwa Serikali itapata mapato mara baada ya kuanza kuuza umeme huo nje ya nchi,ambapo nchi za jirani zinahitaji umeme kwasababu umeme waliokuwa nao ni mdogo na wa gharama kubwa.

Mhe. Majaliwa amesema kuwa faida zote zitakazopatikana zitawanufaisha watanzania wote kwa ujumla na Serikali itasimamia ili kuhakikisha malengo yote yanafikiwa ili ndoto ya baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, aliyekuwa Rais wa Tano Hayati Dkt.John Joseph Magufuli na Rais Mhe Samia Suluhu inatimia.

Hata hivyo, amewataka watanzania waache kubeza mradi huo ambao utakuwa na faida nyingi kwa taifa,na kuwataka watanzania kutembelea mradi ili kujionea wenyewe

# WAZIRI MKUU ARIDHISHWA NA KAZI YA UJENZI WA MRADI WA UMEME WA JULIUS NYERERE





*Mafundi wakiendelea na shughuli za ujenzi mradi wa kufua umeme kwa maji wa Julius Nyerere (JNHPP), Aprili 10,2021.*

maendeleo ya mradi kuliko kusikiliza habari za upotoshaji wa mradi huo.

Pia, amesema malengo ya Serikali kujenga mradi huo, ni kuwa Serikali imedhamiria kupeleka umeme mpaka kwenye vitongoji na kueleza kuwa kazi hiyo ilishaanza na mpaka sasa vijiji vichache tu ndio ambavyo havijapelekewa umeme lakini wakandarasi tayari wapo kwenye maeneo hayo wanaendelea na kazi ya usambazaji umeme vijijini na vitongojini.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato amemueleza Waziri Mkuu kuwa Serikali inamlipa kwa wakati mkandarasi wa mradi huo na mpaka sasa ameshalipwa zaidi ya trilioni 2 ambayo ni asilimia 100 ya kazi yote iliyofanyika mpaka sasa.

Pia, amemuelezea Waziri Mkuu kuwa mradi huo hadi sasa ujenzi wake unaenda vizuri na kwa kasi kubwa na unatarajiwa kukamilika kama ulivyopangwa mwezi Juni 2022.

# WAZIRI WA NISHATI AKABIDHIWA TAARIFA YA MAJADILIANO YA BOMBA LA MAFUTA LA AFRIKA MASHARIKI



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja ambaye pia ni Katibu wa Timu ya Serikali ya Majadiliano ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki, (kushoto) akikabidhi taarifa ya majadiliano ya mradi huo kwa Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kulia).Kulia ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato*

**Na Teresia Mhagama, Dodoma**

Timu ya Serikali ya Majadiliano ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki imekamilisha majadiliano ya mradi huo na kukabidhi Taarifa kwa Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani ikiwa ni ishara ya kuendelea na hatua zaidi ya utekelezaji wa mradi husika.

Taarifa hiyo ilikabidhiwa tarehe 19 Aprili, 2021 na Katibu wa Timu hiyo ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja ambapo viongozi mbalimbali wa Wizara na Taasisi walihudhuria wakiwemo Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Naibu Katibu Mkuu, Kheri Mahimbali, Kamishna wa Petroli na Gesi, Adam Zuberi na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania,(TPDC), Dkt. James Mataragio.

Akizungumza mara baada ya kukabidhiwa Taarifa hiyo, Waziri wa Nishati, alieleza kuwa, majadiliano ya mradi huo yamefanyika kwa takribani miaka mitatu kutokana na ukubwa wa kazi husika na kukamilika kwake kunafungua ukurasa mpya wa kuanza kufanya kazi.

Alisema kuwa, taarifa hiyo inajumuisha masuala mbalimbali ambayo yatapelekea nchi kufaidika na mradi huo ikiwemo masula ya



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akizungumza mara baada ya kukabidhiwa taarifa ya majadiliano ya mradi wa Bomba la Afrika Mashariki. Kulia kwake ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato na kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja ambaye pia ni Katibu wa Timu ya Serikali ya Majadiliano ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki.*

# WAZIRI WA NISHATI AKABIDHIWA TAARIFA YA MAJADILIANO YA BOMBA LA MAFUTA LA AFRIKA MASHARIKI



*Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (kushoto) na Kamishna wa Gesi na Petroli, Adam Zuberi wakiwa katika mkutano na Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani ambao ulihusu makabidhiano ya taarifa ya mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki.*

kikodi, tozo za Serikali, ushiriki wa watanzania katika mradi, fidia, mikataba, bima na masuala ya ardhi.

Pamoja na kuipongeza Timu hiyo ya Majadiliano, Dkt.Kalemani alieleza kuwa jumla ya shilingi bilioni 28.8 zitalipwa kwa watanzania ambao watapisha mradi huo baada ya tathmini kukamilika hivyo ametoa wito kwa wananchi kupisha maeneo ya mradi mara watakapolipwa fidia ili mradi husika utekelezwe kama ilivyopangwa.

Aliongeza kuwa, katika mradi huo yatajengwa makambi 16 pamoja na eneo la kulainisha na kuunganisha vyuma vitakavyotumika kwenye ujenzi ambapo wananchi watakaopisha maeneo hayo pia watalipwa fidia.

Dkt.Kalemani alisema kuwa, katika Bandari ya Tanga, kutajengwa matenki makubwa Matano ambapo mafuta yatakuwa yanashushwa na kazi inayofuata ni kutwaa eneo na kuanza ujenzi baada ya fidia kukamilika.

Kuhusu suala la ajira, Dkt.Kalemani alisema kuwa, jumla ya watanzania 10,000 hadi 15,000 wataajiriwa wakati wa ujenzi wa bomba hilo, na Serikali itahakikisha kuwa watanzania wanaajiriwa kwa zaidi ya asilimia 80 na katika taaluma ambazo watanzania hawana ndipo wataajiriwa watu wa nje ya nchi.

Vilevile alisisitiza watanzania kujiandaa na fursa zitakazotokana na mradi huo ikiwemo utoaji wa huduma mbalimbali kama ulinzi, vifaa vya ujenzi, chakula na usafiri kwa kuwa hatua za ujenzi zitaanza wakati wowote kuanzia sasa.

Alieleza kuwa, Timu maalum itaundwa kwa ajili ya kusimamia mradi huo ambao utajengwa kwa muda wa miaka mitatu na utapita katika mikoa Nane, Wilaya 24 na vijiji zaidi ya 124 hivyo ni watanzania wengi wataguswa na mradi huo na hivyo kufaidika nao.

Aidha, alisema Serikali itafaidika na masuala mbalimbali kutokana na mradi huo kwani Bomba hilo la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki litapitisha takriban mapipa 216,000 ya mafuta kwa siku ambapo kila pipa litalipiwa Dola za Marekani 12.77.



*Watendaji mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati pamoja na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), wakiwa katika mkutano na Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani ambao ulihusu makabidhiano ya taarifa ya mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki.*

# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC) YAMPONGEZA WAZIRI KALEMANI KWA USIMAMIZI MZURI WA MIRADI YA REA



*Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani akiwasilisha Taarifa ya Wizara ya Nishati kuhusu Miradi ya Umeme ya REA mkoani Manyara iliyotembelewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali. Kushoto kwake ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka (mb).*

**Na Dorina G. Makaya – Manyara.**

Kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imempongeza Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani kwa kusimamia vema utekelezaji wa Miradi ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka (mb.) alitoa pongezi hizo kwa niaba ya kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) tarehe 24 mwezi Aprili 2021, mara baada ya wajumbe wa kamati hiyo kutembelea maeneo ya Miradi ya REA hususan kijiji cha Arri na Sigino vilivyoko mkoani Manyara ambapo pamoja na kuunganishwa umeme kwenye kaya, taasisi za elimu na afya pia zimeunganishiwa umeme.

Mwenyekiti huyo wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali Mhe. Naghenjwa Kaboyoka (mb.) alieleza kuwa, kamati yake imeridhishwa na Taarifa ya Utekelezaji ya REA iliyowasilishwa kwao na Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani baada ya kutembelea maeneo husika na kufanya mikutano na wananchi wa vijiji husika vikiwemo Arri na Sigino na kusikia kutoka kwa wananchi wenyewe namna Miradi ya REA ilivyotekelezwa katika vijiji hivyo.

Pia, Kamati hiyo ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, ililisifia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa kutekeleza vema majukumu yake na kuwa mfano wa kuigwa katika nchi nyingine.

Awali akiwasilisha Taarifa ya Wizara ya Nishati kuhusu utekelezaji wa Miradi ya REA, Waziri Kalemani alieleza kuwa, kati ya shule 18 za Sekondari zilizomo katika wilaya ya Babati mjini tayari shule 14 za sekondari zimeunganishiwa umeme na ni shule 4 tu ambazo bado hazijaunganishiwa umeme.

Aidha, Waziri Kalemani alieleza kuwa Kati ya shule za Msingi 56 zilizopo katika Wilaya ya Babati Mjini, tayari shule 24 zimeunganishiwa umeme, na shule 32 zilizobakia zitaunganishiwa umeme mara baada ya taratibu za ujenzi kukamilika.

Akizungumzia kwa Upande wa Wilaya ya Babati Vijijini, Dkt. Kalemani alieleza kuwa, kati ya shule 35 za Sekondari zilizomo



*Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali wakimsikiliza Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani, wakati akiwasilisha Taarifa ya Wizara ya Nishati Kuhusu utekelezaji wa Miradi ya REA mkoani Manyara. (Waziri Kalemani hayumo pichani)*

# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC) YAMPONGEZA WAZIRI KALEMANI KWA USIMAMIZI MZURI WA MIRADI YA REA



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka (mb.) akizungumza na wanakijiji cha Sigino (Hawamo pichani) Kufuatia ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kijijini hapo.*

katika Wilaya ya Babati vijijini, Jumla ya shule za Sekondari 29 tayari zimeunganishiwa umeme na shule 6 zilizobakia zitaunganishiwa umeme. Aidha, amesema, kati ya shule 142 za msingi zilizopo katika Wilaya ya Babati Vijijini tayari shule 56 zimeunganishiwa umeme na zilizobakia pia zitaunganishiwa umeme.

Pia, Dkt. Kalemani alieleza kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuwa, mbali ya kuunganishwa umeme kwenye kaya, taasisi za elimu na afya pia zimeunganishiwa umeme.

Akifafanua kuhusu upatikanaji wa fedha zinazotumika kuendesha Miradi ya REA, Dkt. Medard Kalemani alieleza kuwa, hadi sasa kuna vyanzo vitatu vinavyochangia katika uendeshaji wa Miradi ya REA vikiwemo, Tozo ya asilimia 3 kwenye uzalishaji wa umeme wa biashara kwenye gridi ya Taifa, Tozo ya mafuta; ambapo kwa sasa ni shilingi 100 kwa lita kwenye mauzo ya mafuta ya Petroli na dizeli na shilingi 150 kwa lita ya mafuta ya taa pamoja na michango kutoka kwa wakala na taasisi za fedha za kimataifa na washirika wa maendeleo.

Akijibu swali ni kwa nini mchango wa dizeli ni mdogo ikilinganishwa na mchango wa mafuta ya taa ambayo wananchi wenye kipato kidogo wanatumia, Waziri Kalemani aliweka wazi kuwa, kwa sasa mafuta ya taa hayatumiki kwa wingi ikilinganishwa na mafuta ya Dizeli kwa kuwa tayari Serikali imepeleka umeme vijijini,

Aidha, Waziri Kalemani alikumbushia kuwa, Miradi ya REA haina fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yamepitiwa na miradi ya REA kwani Serikali imelenga kuwafikishia umeme wananchi kwa gharama nafuu sana ya shilingi elfu 27,000 tu na kuwa inatolewa kama huduma kwa wananchi na hakuna mteja yeyote anayetakiwa kulipia nguzo ili kuunganishiwa umeme.

Alisema, kwa wananchi wanaotumia umeme usiozidi unit 75 kwa mwezi wateja hao wanapaswa kulipia shilingi 100 kwa unit na kwa wateja wenye matumizi ya zaidi ya unit 75 wanapaswa kulipia shilingi 294 kwa unit moja.

Pia, Waziri Kalemani alimpongeza Meneja wa TANESCO wa Mkoa wa Manyara Mha. Rehema Mashinji kwa utendaji mzuri na kumtaka kuendelea kusimamia vema kazi ya kuwaunganishia umeme wateja waliolipia kuunganishiwa umeme kwa gharama ya shilingi 27,000 tu.

# Wakongwe kazini rithisheni ujuzi na utaalam kwa vijana wapya

**Na Zuena Msuya**
**Dodoma,**



*Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi, Mhandisi Zena Said, (kulia) na Katibu Mkuu mpya wa Wizara ya Nishati Mhandisi Leonard Masanja (Kushoto), wakisaini nyaraka kabla ya makabidhiano ya ofisi Aprili 27, 2021, jijini Dodoma, wanaoshuhudia ni Naibu katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Kheri Mahimbali (kushoto), na Mkurugenzi wa Huduma za Sheria wa Wizara, Anna Ngowi (katikati)*

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja ametoa wito kwa watumishi wenye ujuzi na uzoefu wa muda mrefu katika sehemu za kazi kurithisha ujuzi walionao kwa watumishi wengine ambao ni vijana ili kuendelea kutekeleza majukumu kwa ufanisi, kwa manufaa ya nchi na Taifa kwa jumla.

Mhandisi Masanja ametoa wito huo, tarehe 27 Aprili, 2021 wakati wa makabidhiano ya ofisi kati yake na Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Katibu wa Baraza la Mapinduzi, Mhandisi Zena Said, ambaye ndiye aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati.



*Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi, Mhandisi Zena Said, (kulia) na Katibu Mkuu mpya wa Wizara ya Nishati Mhandisi Leonard Masanja (Kushoto), wakikabidhiana nyaraka za ofisi wakati wa makabidhiano yaliyofanyika Aprili 27, 2021, jijini Dodoma. Wanaoshuhudia ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara, Kheri Mahimbali (kushoto), na Mkurugenzi wa Huduma za Sheria wa Wizara, Anna Ngowi (katikati).*

Makabidhiano hayo, yalishuhudiwa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali pamoja na Wakuu wa Idara na Vitengo.

Katika makabidhiano hayo, Mhandisi Masanja alieleza kuwa katika utumishi wa umma kila siku watumishi wanastaafu wakiwa na ujuzi na uzoefu hivyo basi, ni vyema wakongwe na wenye ujuzi na uzoefu kuhakikisha wanarithisha utaalamu na ujuzi wao kwa watumishi wengine ili kuendelea kutekeleza majukumu ya Serikali ya kuwahudumia wananchi kwa ufasaha.

"Wakongwe sehemu za kazi na viongozi wa maeneo mbalimbali hakikisheni mnapoondoka katika nafasi hizo, mliowaacha wanawakumbuka kwa mlichokifanya, warithisheni mazuri

# Wakongwe kazini rithisheni ujuzi na utaalam kwa vijana wapya



*Wajumbe wa Menejimenti, wa Wizara ya Nishati, wakimsikiliza Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi, Mhandisi Zena Said, wakati wa hafla ya kukabidhi ofisi kwa Katibu Mkuu mpya wa Wizara hiyo, Mhandisi Leonard Masanja, (kulia kwa Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Said) iliyofanyika Aprili 27, 2021, jijini Dodoma.*

kuwa, tabia hiyo imekuwa ikijenga uadui katika sehemu za kazi, kuweka matabaka na hivyo kuzorotesha utendaji kazi.

Akizungumza na Wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati, Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi, Mhandisi Zena Said, amewaasa viongozi hao wa Menejimenti ya Wizara ya mlionayo, tuache tabia ya kukumbatia ujuzi na uzoefu tulionao na kuacha tabia ya ubinafsi, hii ni kwa faida ya vizazi vyetu vijavyo na Taifa kwa ujumla." alisisitiza Mhandisi Masanja.

Vilevile, aliwaonya baadhi ya viongozi wenye tabia ya kupendelea baadhi ya watumishi katika kugawa majukumu, na kujipendelea wao katika kupata maslahi kuwa kwa kufanya hivyo ni kukiuka taratibu za utumishi wa umma na kwamba mwisho wake ni kuharibu kazi za Serikali.

Masanja pia, alisisiza



*Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu wa Wizara ya Nishati, Ziana Mlawa (aliyesimama) akitoa utambulisho wa wajumbe wa Menejimenti kwa Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi, Mhandisi Zena Said, wakati wa hafla ya kukabidhi Ofisi kwa Katibu Mkuu Mpya wa Wizara, Mhandisi Leonard Masanja, iliyofanyika Aprili 27, 2021.*

# Wakongwe kazini rithisheni ujuzi na utaalam kwa vijana wapya

Nishati kuichukulia kazi kama ni ibada.

Alisema, kufanya hivyo ni kufanya kazi kwa uaminifu huku wakizingatia miongozo na misingi ya kazi bila kumuonea mtu wala kumpendelea mtu kwani nafasi za uongozi, zina fursa kubwa ya kufanya dhuluma ikiwa ni upendeleo kwa watu wasiostahili lakini pia kuwaonea wale ambao wanastahili.

Mha. Zena aliwashauri viongozi hao wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati kutenda kazi kwa uaminifu na si kutenda kwa kutarajia kupata uteuzi wa nafasi za juu jambo linaloweza kuvunja morali ya kazi pale matarajio yao yasipofikiwa.

Amewataka viongozi hao kuwajengea uwezo wa kazi watumishi walio chini yao huku wakiwapa dira ya kutekeleza majukumu yao kitaalam na kiukamilifu.

Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi, Mhandisi Zena Said, amewashukuru viongozi na watumishi wa Wizara ya Nishati kwa ushirikiano waliouonyesha kwake wakati akiwa Katibu Mkuu katika wizara hiyo.

Pia, ametoa wito kwa viongozi na watumishi wa Wizara kufanya kazi kwa kushirikiana na kuheshimiana kwa kuwa, kufanya hivyo kunastawisha utendaji kazi na kuwezesha kufanya kazi kwa kasi, ubunifu na kwa usahihi.

Sambamba na hilo ameupongeza uongozi wa Wizara ya Nishati pamoja na watumishi wake kwa kazi nzuri zinazoendelea kufanyika za kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo Umeme na Gesi.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Wizara, Kheri Mahimbali, amemueleza Mhandisi Zena Said kuwa, wataendelea kushirikiana na ofisi yake katika kuwahudumia wananchi katika Sekta ya Nishati.

Hata hivyo, Mahimbali amemuomba Mhandisi Zena Said kushirikana katika utatuzi wa changamaoto zozote zilizopo na zinazoweza kujitokeza katika sekta ya Nishati kwa kuwa Bara na Visiwani ni nchi moja, na amemuomba aendelee kuwa Balozi mzuri katika kuiwakalisha Tanzania kwenye sekta hiyo.



*Katibu Mkuu, Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi, Mhandisi Zena Said, akiwa katika picha ya pamoja na Katibu Mkuu mpya wa Wizara ya Nishati Mhandisi Leonard Masanja (mbele Kulia), Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Kheri Mahimbali (mbele kushoto), na Menejimenti ya Wizara hiyo, wakati wa hafla ya kukabidhi ofisi ya Katibu Mkuu iliyofanyika Aprili 27,2021, jijini Dodoma.*

# Bei ya kuunganishiwa umeme Dodoma ni shilingi 27,000 tu



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (pili kushoto) akikagua kazi ya usambazaji umeme katika Kata ya Ntyuka jijini Dodoma. Wengine katika picha ni Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini, Antony Mavunde ( kulia), na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini ( REA) Mhandisi Jones Olotu(pili kulia) watendaji kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wizara ya Nishati, iliyofanyika Aprili 01, 2021.*

**Na Zuena Msuya, Dodoma**

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani amesema kuwa, maeneo yote ya Mkoa wa Dodoma yataunganishiwa umeme kwa gharama ya shilingi ya 27,000 tu na si zaidi ya hapo.

Dkt. Kalemani amesema hayo wakati wa ziara yake ya kikazi ya kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme katika baadhi ya maeneo ya mitaa ya Mkoa wa Dodoma ikiwemo iliyopo katika Kata ya Ntyuka iliyofanyika Aprili 01, 2021.

"Nimefanya ziara ya kujiridhisha kuona kwa nini wananchi wengi hawaunganishi umeme,nikagundua kuwa moja ya sababu ni bei kubwa ya kuunganisha umeme, na maeneo mengi ya makazi ya Dodoma ni kama vijiji hivyo, mradi wa usambazaji wa umeme vijijini ulikuwa katika mkoa huu hata





*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kushoto) akizungumza na wakazi wa Kata ya Ntyuka wakati alipokuwa akikagua kazi ya usambazaji umeme katika Kata ya Ntyuka jijini Dodoma. Wengine katika picha ni Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini, Antony Mavunde (pili kushoto), iliyofanyika Aprili 01, 2021.*

# Bei ya kuunganishiwa umeme Dodoma ni shilingi 27,000 tu



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akizungumza na wakazi wa Kata ya Ntyuka wakati alipokuwa akikagua kazi ya usambazaji umeme katika Kata ya Ntyuka jijini Dodoma. Wengine katika picha ni Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini, Antony Mavunde (pili kushoto), iliyofanyika Aprili 01, 2021.*

kabla ya kuwa Makao Makuu ya nchi, hivyo naagiza wakandarasi pamoja Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kuhakikisha wakazi wa mkoa huu wote wanaunganishiwa umeme kwa shilingi 27,000, pasipo kuruka nyumba wala kuzibagua." alisema Kalemani.

Kwa mantiki hiyo, amewataka wananchi wote ambao wametandaza nyaya katika nyumba zao kulipia gharama hizo haraka iwezekanavyo ili kuunganishiwa umeme.

Ameeleza kuwa, awali baadhi ya maeneo ya Mji wa Dodoma yalikuwa yakiunganishiwa umeme kwa zaidi ya shilingi Laki tatu.

Aidha, ameagiza kuwa, transfoma ziongezwe kwenye maeneo mbalimbali nchini kwani inapofungwa transfoma moja katika eneo lenye makazi mengi, inapelekea umeme kukatika mara kwa mara.

Katika hatua nyingine, Waziri wa Nishati amesema kuwa, ukarabati wa mitambo mbalimbali ya umeme nchini umekamilika hivyo hatarajii kuona umeme ukikatika mara kwa mara na kwamba ikiwa kuna Meneja wa Wilaya ambaye katika eneo lake umeme unakatika mara kwa mara, ndani ya siku 15 atatoa maelekezo ya kuwabadilisha Mameneja na wengine kushushwa vyeo.

Kuhusu umeme Vijijini, alieleza kuwa, wananchi ambao bado hawajasambaziwa umeme, watapata nishati hiyo ndani ya miezi 18, pia vitongoji navyo vimeshaanza kusambaziwa umeme na kazi husika itakamilika ndani ya miaka Miwili.

Vilevile ametoa msisitizo wa watendaji husika kuwa hataki kuona nguzo za umeme zimelala chini na badala yake zisimikwe katika maeneo yanayohitaji nguzo hizo.

# Uwekaji vinasaba kwenye mafuta ufanyike kwenye matenki - Dkt.Kalemani



*Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani (wa Pili kushoto) akikagua kazi ya uwekaji vinasaba kwenye ghala la mafuta la kampuni ya Camel Oil mkoani Dar es Salaam. Wa kwanza kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dkt. Athuman Ngenya*

**Na Teresia Mhagama, Dar es Salaam**

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani ameliagiza Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kuhakikisha kuwa uwekaji wa vinasaba kwenye mafuta kama vile petroli na dizeli unafanyika kuanzia kwenye matenki yanayohifadhi mafuta hayo badala ya magari ili kuhakikisha kuwa mafuta yote yanayosambazwa nchini yanakuwa na ubora na Serikali inapata kodi stahiki.

Dkt.Kalemani alitoa agizo hilo tarehe 28 Aprili, 2021 mara baada ya kufanya ziara kwenye maghala ya mafuta ya kampuni za Camel Oil na Oil Com, Kurasini mkoani Dar es Salaam na kukuta wataalam kutoka TBS wakifanya kazi ya uwekaji wa vinasaba kwenye magari ya kusafirisha mafuta ya kampuni tajwa.

"Nataka muanze kupima mafuta kuanzia kwenye matenki yenyewe, hadi kwenye vituo, siyo tu kusubiri pale wanapopakia kwenye magari, Je ikitokea wamepakia wakati hampo, mtajuaje kuwa mafuta husika yana ubora?"Alisema Dkt. Kalemani

Dkt.Kalemani alieleza kuwa, amefanya ukaguzi wa kazi ya uwekaji wa vinasaba kwenye mafuta ili kujiridhisha kama TBS wanafanya kazi husika kwa ufanisi baada ya kukabidhiwa kutekeleza jukumu hilo ambalo awali lilikuwa likifanywa na mkandarasi binafsi ambaye alikuwa akilipwa takriban shilingi Bilioni Tano kwa mwezi.

Aliongeza kuwa, Serikali imekuwa ikipoteza fedha nyingi kumlipa mkandarasi binafsi kuweka vinasaba kwenye mafuta badala ya TBS ambayo ndiyo yenye dhamana ya kuhakikisha kuwa mafuta yanayouzwa nchini yanakuwa na ubora stahiki.

"Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa, mafuta yanakuwa na




*Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani (kushoto) akizungumza na wataalam kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na kampuni ya Camel Oil mara baada ya kukagua kazi ya uwekaji vinasaba kwenye ghala la mafuta la kampuni ya Camel Oil mkoani Dar es Salaam.*

# Uwekaji vinasaba kwenye mafuta ufanyike kwenye matenki - Dkt.Kalemani



*Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani (wa Tatu kushoto) akiwa katika ghala la mafuta la kampuni ya Camel Oil wakati alipofika kukagua kazi ya uwekaji vinasaba kwenye ghala hilo mkoani Dar es Salaam. Wa Pili kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dkt. Athuman Ngenya.*

ina jukumu la kupima mafuta hayo na EWURA ndiye mwenye jukumu la kumsimamia mpimaji.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dkt. Athuman Ngenya alimhakikishia Waziri wa Nishati kuwa, TBS ina uwezo wa kufanya kazi ya uwekaji vinasaba kwenye magari na kwamba mafuta yote yanayosambazwa nchini yanakuwa na vinasaba.

Katika ziara yake kwenye maghala hayo ya mafuta mkoani Dar es Salaam, Waziri wa Nishati aliambatana na Kaimu Kamishna wa Petroli na Gesi, Sebastian Shana, na Wakuu wa Taasisi za Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA), TBS na EWURA.

ubora, kodi zinapatikana na pia tunajenga uwezo wa watu wetu kufanya kazi husika na Taasisi zetu zisimamie kazi hii badala ya kutegemea watu kutoka nje ya nchi." Alisisitiza Dkt.Kalemani

Katika ukaguzi huo, Dkt.Kalemani aliiagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), kuhakikisha kuwa, wanasimamia kikamilifu kazi ya uwekaji wa vinasaba kwenye mafuta nchini kwani TBS




*Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani (wa Tatu kulia) akiwa katika ghala la mafuta la kampuni ya Oil Com wakati alipofika kukagua kazi ya uwekaji vinasaba kwenye ghala hilo mkoani Dar es Salaam. Wengine katika picha ni watendaji kutoka Wizara ya Nishati, Taasisi za Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA), TBS na EWURA*

# KATIBU MKUU NA NAIBU KATIBU MKUU WIZARA YA NISHATI WAANZA KAZI RASMI

- ***Wasisitiza Uadilifu, Bidii na Uaminifu***



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja akisaini kitabu mara baada ya kuwasili katika Ofisi za Wizara ya Nishati Mtumba jijini Dodoma.*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja na Naibu Katibu Mkuu, Kheri Abdul Mahimbali wakiwa katika mazungumzo mara baada ya kuwasili katika Ofisi za Wizara ya Nishati, Mtumba jijini Dodoma.*

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja na Naibu Katibu Mkuu, Kheri Abdul Mahimbali, tarehe 8 Aprili, 2021, wameanza kazi rasmi katika Wizara ya Nishati baada ya kuapishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, kushika nyadhifa hizo April 6, 2021.

Baada ya kuwasili katika Ofisi za Wizara ya Nishati, viongozi hao walifanya mazungumzo na Menejimenti ya Wizara pamoja na watumishi.

Akizungumza na Menejimenti ya Wizara pamoja na Watumishi, Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja amewataka kufanya kazi kwa bidii, uaminifu na



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja akizungumza na Menejimenti na baadhi ya watumishi wa Wizara mara baada ya kuwasili katika Ofisi za Wizara ya Nishati, Mtumba jijini Dodoma. Kushoto kwake ni Naibu Katibu Mkuu, Kheri Abdul Mahimbali na wa kwanza kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Daniel Machunda.*



*Kamishna wa Petroli na Gesi, Adam Zuberi akizungumza wakati Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja na Naibu Katibu Mkuu, Kheri Abdul Mahimbali walipofanya kikao na Menejimenti na baadhi ya watumishi wa Wizara mara baada ya kuwasili katika Ofisi za Wizara ya Nishati, Mtumba jijini Dodoma.*

# KATIBU MKUU NA NAIBU KATIBU MKUU WIZARA YA NISHATI WAANZA KAZI RASMI

uadilifu.

Aidha, amewataka watumishi hao kufanya kazi kwa ushirikiano ili Wizara iweze kufanikisha shughuli zake zote, na malengo yaliyopangwa yaweze kutekelezeka kwa urahisi.

Vilevile, amewataka Wakuu wa Idara na Vitengo, kuwa wabunifu ili kuongeza ufanisi katika majukumu yao, na pia kuwawezesha watumishi waliopo chini yao ili wafanye majukumu yao kwa ufanisi.

Pia amewataka Wakuu hao wa Idara na Vitengo, kuweka usawa katika mgawanyo wa majukumu ili kila mtumishi aweze kuwatumikia watanzania kwa nafasi aliyonayo.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu, wa Wizara ya Nishati, Kheri Abdul Mahimbali, amewataka watumishi wa Wizara kufanya kazi kwa ushirikiano na kuahidi kutumia uzoefu wake katika sekta ya Nishati ili kufanikisha majukumu ya Wizara.



*Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Abdul Mahimbali akizungumza na Menejimenti na baadhi ya watumishi wa Wizara mara baada ya kuwasili katika Ofisi za Wizara ya Nishati, Mtumba jijini Dodoma. Kulia kwake ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja na kushoto kwake ni ni Kaimu Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Daniel Machunda.*



*Kaimu Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Daniel Machunda akizungumza wakati Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard na Naibu Katibu Mkuu, Kheri Abdul Mahimbali walipowasili katika Ofisi za Wizara ya Nishati, Mtumba jijini Dodoma.*



*Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Abdul Mahimbali akisaini kitabu mara baada ya kuwasili katika Ofisi za Wizara ya Nishati Mtumba jijini Dodoma. Kulia ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard.*

# MAMENEJA TANESCO WATAKIWA KUJIPANGA UPYA

**Hafsa Omar-Dodoma**

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani amewataka Mameneja wa Shirika la Umeme Tanzania ( TANESCO), nchi nzima, kujipanga upya na kuhakikisha kuwa wanafanyakazi kwa kasi, ubunifu na kuzingatia weledi ili waweze kuboresha mapungufu yote yanayojitokeza katika kazi za uzalishaji, uunganishaji na usambazaji umeme.

Alisema hayo wakati wa kikao chake na Mameneja wa TANESCO na Wasimamizi wa Miradi ya Wakala wa Nishati vijijini wa kanda (REA) kilichofanyika tarehe 25 Aprili 2021, jijini Dodoma na kuhudhuriwa na Naibu Waziri wa Nishati Wakili, Stephen Byabato, Naibu katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali, Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu Edward Ishengoma, Mkurugenzi Mtendaji TANESCO, Dkt. Tito Mwinuka na wataalam mbalimbali kutoka katika Wizara ya Nishati na Taasisi zake.

Alisema, lengo la Serikali ni kuona umeme wa gridi ya taifa unaunganishwa katika mikoa yote nchini ili watanzania wote wapate umeme wa uhakika na kuwataka mameneja ambao mikoa yao haipo kwenye gridi kuanza kufanyia kazi mara moja suala hilo.

Pia, aliwaagiza Mameneja hao kupeleka umeme kwa wananchi bila kuchelewa, " ile tabia ya wananchi wameshalipa pesa kwa ajili ya kuunganishiwa umeme



*Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani akizungumza kwenye kikao na Mameneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wasimamizi wa Miradi ya Wakala wa Nishati vijijini wa kanda(REA) kilichofanyika jijini Dodoma Aprili 25,2021.*



*Naibu Waziri wa Nishati Wakili, Stephen Byabato akizungumza kwenye kikao na Mameneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wasimamizi wa Miradi ya Wakala wa Nishati vijijini wa kanda (REA) na washiriki mbalimbali, kilichofanyika jijini Dodoma Aprili 25,2021.*



*Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani (katikati), Naibu Waziri wa Nishati Wakili, Stephen Byabato (kulia), Naibu katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Abdul Mahimbali (kushoto) wakiwa kwenye kikao na Mameneja wa Shirika la Umeme Tanzania(TANESCO) na Wasimamizi wa Miradi ya Wakala wa Nishati vijijini wa kanda(REA) kilichofanyika jijini Dodoma Aprili 25,2021.*

# MAMENEJA TANESCO WATAKIWA KUJIPANGA UPYA



*Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu wa Wizara ya Nishati, Bi Ziana Mlawa akiwa katika kikao baina ya Waziri wa Nishati na Mameneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wasimamizi wa Miradi ya Wakala wa Nishati vijijini wa kanda(REA) kilichofanyika jijini Dodoma Aprili 25,2021.*

halafu wanachukua muda mrefu kufuatilia kuanganishiwa umeme bila mafanikio isijitokeze tena".Alisisitiza

Aidha, aliwataka kuendelea kukusanya mapato ya Shirika hilo,ikiwa ni pamoja na kukusanya madeni ya wadaiwa sugu, ili Shirika hilo liendee kujitegemea na kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi, hata hivyo aliwapongeza kwa juhudi zao za kukusanya mapato ambapo kwa sasa wanakusanya zaidi ya shilingi billioni 40 kwa wiki.

Waziri Kalemani, pia aliwataka kuhakikisha kuwa miradi yote inakamilika kwa wakati ikiwemo mradi mkubwa wa kufua Umeme kwa Maji wa Julius Nyerere(JNHPP) pamoja na miradi yote ya REA.

"Nataka miradi yote ikamilike, na ndani ya miezi 18 nataka vijiji vyote viwe vimeshapelekewa umeme, kila meneja ahakikishe vijiji kwenye eneo lake vipo kwenye mpango na Desemba mwakani vijiji vyote viwe vimepelekewa umeme."alisema

Pia, aliwataka kuendelea kutoa huduma bora kwa wateja na kuwa na mahusiano mazuri na wateja hao katika maeneo yao ya kazi.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nishati Wakili, Stephen Byabato,aliwapongeza TANESCO kwa kufanya kazi nzuri ya usambazaji umeme nchini na kuwataka kuendelea kufanya kazi kwa juhudi kwakuwa kazi yote nzuri inayoonekana ni kwa sababu ya juhudi hizo na usimamizi mzuri wa Wizara ya Nishati.







*Washiriki mbalimbali wakiwa katika kikao baina ya Waziri wa Nishati na Mameneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wasimamizi wa Miradi ya Wakala wa Nishati vijijini wa kanda(REA) kilichofanyika jijini Dodoma Aprili 25,2021.*

# Marufuku kuagiza Vikombe (Insulators) kutoka nje ya Nchi -Dkt.Kalemani

**Na Teresia Mhagama, Dar es Salaam**



*Mashine Tatu kati ya Nne zilizopo katika kiwanda cha Inhemeter ambazo hutengeneza vikombe (insulators) zinazotumika kwenye miundombinu ya usafirishaji na usambazaji umeme.*

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani amepiga marufuku uagizaji wa vikombe (insulators) kutoka nje ya nchi baada ya uzalishaji wa vikombe hivyo sasa kufanyika nchini.

Dkt.Kalemani ametoa agizo hilo tarehe 28 Aprili, 2021 baada ya kukagua shughuli za uzalishaji wa vikombe hivyo katika Kiwanda cha Inhemeter kilichopo wilayani Kinondoni mkoani Dar es Salaam.

"Nilikuja hapa mwezi Novemba mwaka jana kukagua uzalishaji wa mita za umeme na nikatoa agizo kuwa vikombe navyo visiagizwe nje ya nchi na viwanda vya uzalishaji wa vikombe vijengwe ndani ya nchi, hivyo nimekuja kufuatilia agizo hilo na kujiridhisha kama vikombe vinazalishwa au havizalishwi." Amesema Dkt.Kalemani



*Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani akiwa ameshika moja ya vikombe (insulators) vinavyozalishwa katika kiwanda cha Inhemeter jijini Dar es Salaam.Kulia kwake ni Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Amos Maganga na wengine ni watendaji kutoka Wizara ya Nishati, TANESCO na kiwanda cha Inhemeter.*

Baada ya kufanya ukaguzi katika kiwanda hicho, Dkt. Kalemani amesema kuwa, amejiridhisha kuwa kiwanda kinazalisha vikombe takriban milioni 1.5 kwa mwaka na pia kiwanda kingine cha Africab kinazalisha vikombe Milioni Moja kwa mwaka huku mahitaji kwa sasa yakiwa ni vikombe Milioni M1.8.

Kutokana na uzalishaji huo, Dkt.Kalemani ameeleza kuwa Shirika la Umeme Tanzania

# Marufuku kuagiza Vikombe (Insulators) kutoka nje ya Nchi -Dkt.Kalemani

(TANESCO), Wakala wa Nishati Vijijini (REA) pamoja na wakandarasi wa umeme wanunue vikombe na vifaa vingine vya umeme vinavyozalishwa ndani ya nchi, hali itakayopelekea wananchi kuunganishiwa umeme kwa kasi.

Ameeleza kuwa, kuna faida mbalimbali za kuzalisha vifaa hivyo ndani ya nchi ikiwemo vifaa husika kupatikana kwa bei nafuu kulinganisha na vifaa vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi, vifaa hivyo kutengenezwa kwa ubora na kuongeza ajira ndani ya nchi.

Aidha, ameipongeza kampuni hiyo kwa kuzalisha vifaa hivyo na kutoa ajira kwa vijana wa kitanzania takriban 150.

Ametoa wito kwa watendaji wa kiwanda hicho kuongeza uzalishaji wa vikombe hivyo ambavyo hufungwa katika miundombinu ya usafirishaji na usambazaji umeme ya uwezo tofauti ikiwemo 11kV, 33kV na 400kV.

Insulators (vikombe) hufungwa kati ya nguzo na nyaya za umeme kwa lengo la kuzuia umeme huo kusafiri kupitia kwenye nguzo na baadaye kuleta madhara mbalimbali ikiwemo ya moto.

Katika ziara yake jijini Dar es Salaam, Waziri wa Nishati aliambatana na watendaji mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati, Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).



*Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani akiangalia moja ya mashine kati ya Nne zilizopo katika kiwanda cha Inhemeter ambazo hutengeneza vikombe (insulators) zinazotumika kwenye miundombinu ya usafirishaji na usambazaji umeme.Kulia kwake ni Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Amos Maganga na wengine ni watendaji kutoka Wizara ya Nishati, TANESCO na kiwanda cha Inhemeter.*



*Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani akiwa ameshika moja ya vikombe (insulators) vinavyozalishwa katika kiwanda cha Inhemeter jijini Dar es Salaam.Kulia kwake ni Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Amos Maganga na wengine ni watendaji kutoka Wizara ya Nishati, TANESCO na kiwanda cha Inhemeter.*



*Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani akiangalia baadhi ya vifaa katika kiwanda cha Inhemeter ambacho hutengeneza vikombe (insulators) zinazotumika kwenye miundombinu ya usafirishaji na usambazaji umeme. Wa pili kushoto ni Kaimu Kamishna wa Petroli na Gesi, Sebastian Shana na Kulia kwa Waziri ni Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Amos Maganga na wengine ni watendaji kutoka Wizara ya Nishati, TANESCO na kiwanda cha Inhemeter.*

# MEI MOSI










*Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati waliposhiriki Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani ambayo huadhimishwa kila tarehe moja ya mwezi wa Tano kila mwaka. Maadhimisho hayo yalifanyika katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma ambapo kitaifa yalifanyika mkoani Mwanza.*

*Kauli mbiu ya Maadhimisho hayo ni **MASLAHI BORA, MISHAHARA JUU, KAZI IENDELEE,** huku Wizara ya Nishati ikiunga mkono kauli mbiu hiyo kwa kusema **"Kasi ya utoaji huduma za Nishati iendelee".***

# JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI




*Fika Ofisi ya Mawasiliano,*
**Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au**
Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018
**Nukushi** +255-26-2320148

*www.nishati.go.tz*
*Wizara ya Nishati*
*@Nishati2017*
*wizara_ya_nishati_tanzania*
*Wizara ya Nishati*